

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 61 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** MACHI 2026

TSC YASIKILIZA NA KUAMUA RUFAA 39 ZA WALIMU



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama akitoa taarifa ya rufaa zilizoamuliwa na Tume wakati wa kuhitimisha Mkutano wa Tume mjini Morogoro hivi karibuni.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

 Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania  [tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

Rufaa za Walimu ziendelee kuwa Somo la Maadili na Uwajibikaji

Hatua ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kusikiliza na kuamua rufaa za walimu wanaopinga maamuzi ya Mamlaka za Nidhamu ngazi ya wilaya inapaswa kuwa somo kwa wadau wote wa elimu. Hivi karibuni Tume imeamua rufaa 39 za walimu ambapo miongoni mwa hizo, zipo zilizokataliwa kwa kuwasilishwa nje ya muda wa kisheria, zipo zilizorejeshwa kuanza upya kutokana na dosari za kiutaratibu, na nyingine kuthibitishwa au kutenguliwa. Haya yote yanaonesha kuwa nidhamu na ufuataji wa taratibu ni jambo lisiloweza kupuuzwa katika taaluma ya ualimu.

Rufaa zilizokataliwa kwa kuchelewa kuwasilishwa zinatoa fundisho muhimu kuwa kuzijua na kuziheshimu Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu ni kinga kwa mwalimu. Tunatoa wito kwa walimu wote kuwa makini na mienendo yao kazini na katika jamii, na pia kufahamu haki na wajibu wao kwa wakati. Nidhamu, uadilifu na uwajibikaji ni silaha bora ya kujiepusha na mashauri ya kinidhamu yanayoweza kuathiri taaluma na maisha binafsi.


Kwa upande mwingine, rufaa zilizorejeshwa kutokana na dosari katika uendeshaji wa mashauri

zinaikumbusha Mamlaka za Nidhamu umuhimu wa kuzingatia taratibu kwa umakini. Tunaziomba mamlaka hizo kutekeleza wajibu wao kwa haki, bila upendeleo na kwa kuzingatia misingi ya ushahidi na haki. Kila shauri linapaswa kuendeshwa kwa umakini ili kuepusha makosa yanayoweza kusababisha rufaa kushinda au kurejeshwa, hali inayoweza kuigharimu Serikali muda na rasilimali fedha.

Ni wajibu wa Wakuu wa Shule na Kamati za Wilaya kutambua kuwa mamlaka waliyopewa ni dhamana ya kusimamia maadili na kulinda maslahi ya taasisi, si chombo cha kuonea au kuamua bila kuzingatia sheria. Tunatoa wito kwao kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu wakati wote ili kuhakikisha haki inatendeka kwa pande zote.

Kuimarisha nidhamu katika sekta ya elimu ni jukumu la pamoja. Walimu wajitathmini na kujenga utamaduni wa maadili mema na mamlaka za nidhamu zisimamie sheria kwa uwazi na weledi ili Tume iendelee kuwa msimamizi wa haki. Pale maadili, sheria na haki vinapokutana, taaluma ya ualimu huimarika, heshima yake hulindwa na mchango wake kwa Taifa huwa wenye tija.

KATUNI



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Paulina M. Nkwama

Wajumbe
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya
Edwin Mgendera
Apsa Othman
Asha Lubuva

Mhariri Mkuu
Artemony T. Vincent

Mhariri
Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa
Lucas G. Ogunde

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**



TSC YASIKILIZA NA KUAMUA RUFEE 39 ZA WALIMU



Mwenyekiti wa Tume, Prof. Masoud Muruke akihitimisha Mkutano wa Tume uliofanyika mjini Morogoro hivi karibuni.

Na Mwandishi Wetu – Morogoro

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imesikiliza na kuamua rufaa 39 zilizowasilishwa na walimu waliokata rufaa kupinga maamuzi ya Mamlaka za Nidhamu ngazi ya wilaya.

Taarifa hiyo ilitolewa hivi karibuni na Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama, wakati wa majumuisho ya mkutano wa siku tano wa Tume uliofanyika katika Ukumbi wa Magadu, mjini Morogoro.

Akitoa ufafanuzi wa maamuzi hayo, alisema kuwa kati ya rufaa 39 zilizopitiwa, rufaa 15 zilikataliwa kwa kuwa ziliwasilishwa nje ya muda wa kisheria wa siku 45 tangu mwalimu kupokea uamuzi wa shauri lake.

Aidha, rufaa saba (7) zilirejeshwa katika Mamlaka za Nidhamu ngazi ya wilaya ili zianzishwe upya kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu baada ya kubainika kuwepo kwa dosari katika mwenendo wa mashauri hayo.

Kwa upande mwingine, rufaa nane (8) zilikubaliwa, ambapo Tume ilitengua maamuzi ya Kamati za Wilaya za Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo. Hata hivyo, katika rufaa tisa

(9), Tume ilikubaliana na maamuzi ya kamati hizo na kuthibitisha adhabu zilizotolewa.

Katibu huyo alieleza kuwa Tume itaendelea kuwasiliana na mamlaka za shule zenye changamoto za nidhamu ili kudhibiti vitendo vinavyosababisha walimu kuingia katika mashauri ya kinidhamu. Aliongeza kuwa Menejimenti ya Tume, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, itaendelea kutoa elimu kwa walimu kuhusu umuhimu wa kuzingatia maadili ya taaluma ili kulinda hadhi ya ualimu.

Naye Kamishna wa Tume, Bw. Lameck Philipo Mahewa, aliishauri Menejimenti kufanya uchambuzi wa takwimu za walimu wa shule za msingi na sekondari za umma ili kubaini idadi ya watakaostaafu kwa hiari, kwa lazima au kwa sababu nyinginezo, hatua itakayosaidia katika mipango ya rasilimali watu.

Pia alisisitiza haja ya kuendelea kuwajengea uwezo Wakuu wa Shule kama Mamlaka ya Kwanza ya Nidhamu, ili watekeleze majukumu yao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu bila kutumia vibaya mamlaka waliyopewa.

“Wapo Wakuu wa Shule ambao,


kwa kujua au kutojua, wanaweza kutumia mamlaka waliyopewa kama chombo cha kuwakandamiza wengine. Ni muhimu wakapatiwa elimu ya kutosha ili watekeleze wajibu wao kwa weledi na kwa kuzingatia mipaka ya mamlaka yao,” alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Tume, Prof. Masoud Hadi Muruke, aliagiza Menejimenti ya Tume kukutana mara kwa mara na Kamati za Wilaya za Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo kwa lengo la kuzikumbusha kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu katika uendeshaji wa mashauri ya walimu.

Alisema hatua hiyo itasaidia kupunguza dosari zinazojitokeza katika mashauri, ambazo wakati mwingine husababisha rufaa kushinda au kurejeshwa kuanza upya na hivyo kuisababishia Serikali hasara.

Katika mkutano huo wa siku tano, mada mbalimbali ziliwasilishwa ikiwemo Mpango wa Bajeti kwa kipindi cha Robo ya Kwanza (Julai–Septemba) 2025/26, Rasimu ya Mpango Mkakati wa Tume wa mwaka 2026/27–2030/31 pamoja na taarifa za wenyevidi wa kamati za Tume.

TSC YASIKILIZA NA KUAMUA RUFAA 39 ZA WALIMU



Washiriki wa Mkutano wa Tume wakizwa kwenye mkutano huo uliofanyika hivi karibuni mjini Morogoro.

TSC YAIMARISHA UTOAJI HUDUMA KWA KUTUMIA MFUMO WA KIELEKTRONIKI (TSCMIS)



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama, akiwasilisha mada kuhusu matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utekelezaji wa shughuli za TSC nchini wakati wa Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili wa Umoja wa Maafisa Elimu Mikoa na Halmashauri (REDEOA) uliofanyika jijini Arusha.

Na Mwandishi Wetu

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imefanikiwa kujenga Mfumo wa Kielektroniki wa Teachers Service Commission (TSCMIS) ambao umewezesha upatikanaji wa taarifa sahihi za walimu na kurahisisha ushughulikiaji wa masuala ya nidhamu na malalamiko kwa haraka na kwa ufanisi.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama, alipokuwa akiwasilisha mada kuhusu matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utekelezaji wa shughuli za TSC nchini wakati wa Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili wa Umoja wa Maafisa Elimu Mikoa na Halmashauri (REDEOA) uliofanyika jijini Arusha.

Alisema mfumo huo umeboresha utoaji wa huduma kwa walimu kwa wakati na kwa ufanisi, umerahisisha mchakato wa kushughulikia mashauri

ya nidhamu na rufaa kuanzia ngazi ya shule, wilaya hadi Makao Makuu, pamoja na kurahisisha utoaji wa namba za usajili kwa walimu (TSC Number).

Mwl. Nkwama alieleza kuwa mfumo huo unawawezesha walimu kupata huduma wakiwa katika vituo vyao vya kazi na kuwaondolea usumbufu wa kufuata huduma katika ofisi za Tume ngazi ya wilaya. Aidha, umeisaidia Tume kupata taarifa kwa wakati na kwa usahihi.

Aliongeza kuwa mfumo huo unatumika katika shughuli mbalimbali, ikiwemo usajili wa walimu, usimamizi wa mashauri, na unamwzesha mwalimu kukata rufaa kwa njia ya kielektroniki huku mamlaka husika zikishughulikia rufaa hizo kupitia mfumo huo.

Faida nyingine za TSCMIS ni pamoja na usimamizi wa maswali kupitia Dawati la Huduma na ukokotoaji wa mafao kwa walimu waliohitimisha ajira kabla ya mwaka

2004, kabla ya kuanza kwa mifuko ya hifadhi ya jamii, pamoja na walimu wa ajira za mikataba ambao malipo yao hufanywa na Hazina.

Mwl. Nkwama alibainisha kuwa TSCMIS imeunganishwa na mifumo mingine ya Serikali kwa ajili ya kubadilishana taarifa na kukamilisha mchakato ya kiutumishi, ikiwemo eWatumishi (HCMIS), SIS ya TAMISEMI na TPPS ya Hazina.

Alifafanua kuwa mfumo wa eWatumishi (HCMIS) husaidia kupata taarifa binafsi za mwalimu, historia ya upandishaji madaraja, mabadiliko ya miundo pamoja na taarifa za kitaaluma.

Kwa upande wa SIS (TAMISEMI), alisema mfumo huo husaidia kupata taarifa za mahudhurio ya mwalimu, masomo anayofundisha na kituo chake cha kazi, huku TPPS (Hazina) ukirahisisha mchakato wa malipo ya pensheni na mirathi kwa walimu wanaolipwa na Hazina.

DKT. MWINYI AWEKA MSISITIZO WA MAADILI NA UWAJIBIKAJI KWA WALIMU AJIRA MPYA BUSOKELO

Na Mwandishi wetu – Busekelo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo, Dkt. Mwinyi Mwinyi, amewataka walimu wa ajira mpya kufanya kazi kwa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma, uwajibikaji na uzalendo ili kuimarisha sekta ya elimu katika halmashauri hiyo.

Akifungua mafunzo elekezi yaliyofanyika Februari 26, 2026 katika makao makuu ya halmashauri, Dkt. Mwinyi aliwakaribisha rasmi walimu 23 wa kada ya Elimu ya Sekondari waliopangiwa kuanza kazi Busokelo, akieleza kuwa ujio wao ni nyongeza muhimu katika juhudi za kuinua viwango vya ufaulu na nidhamu shuleni.

Katika hotuba yake, Dkt. Mwinyi alisisitiza kuwa taaluma ya ualimu si ajira ya kawaida bali ni wito unaohitaji kujitolea, uvumilivu na moyo wa huduma kwa jamii. Alieleza kuwa mwalimu ana nafasi ya kipekee katika malezi ya kizazi cha sasa na kijacho, hivyo anapaswa kuwa mfano bora wa kuigwa katika mwenendo, maamuzi na maisha yake ya kila siku.

“Ualimu ni kada iliyo karibu sana na jamii. Walimu ni kioo cha



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo, Dkt. Mwinyi Mwinyi akizungumza na walimu wapya ajira mpya wakati wa ufunguzi wa mafunzo elekezi yaliyofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, tarehe 26 Februari, 2026.

jamii, hivyo mnapaswa kuishi kwa nidhamu, uadilifu na heshima ili jamii iwaheshimu na kuwaamini,” alisisitiza.

Aidha, aliwakumbusha walimu hao umuhimu wa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa

Umma pamoja na kuepuka vitendo vinavyoweza kuchafua taswira ya taaluma hiyo, ikiwemo uzembe, uoro, matumizi mabaya ya pombe na kujiingiza katika makundi yasiyofaa. Alisisitiza kuwa maadili mema na nidhamu kazini ni msingi wa mafanikio ya mtumishi na taasisi kwa ujumla.

Dkt. Mwinyi pia aliwahimiza walimu hao kujiendeleza kitaaluma, kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji na kuzingatia mahitaji ya wanafunzi ili kuongeza uelewa na ufaulu. Alieleza kuwa halmashauri itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika, lakini walimu nao wanapaswa kuonesha bidii, ubunifu na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu yao.

Kwa upande wao, baadhi ya walimu walioshiriki mafunzo hayo walieleza kuwa wamepokea maelekezo yaliyotolewa na wako tayari kuanza majukumu yao kwa ari mpya, wakiahidi kushirikiana na uongozi wa shule na jamii kwa ujumla ili kufikia malengo ya kielimu katika Wilaya ya Busokelo.

Mafunzo hayo elekezi yamelenga kuwajengea walimu uelewa kuhusu mazingira ya kazi, wajibu wao kama watumishi wa umma na matarajio ya halmashauri katika kuboresha sekta ya elimu.



Mmoja wa walimu ajira mpya akitoa maoni na kuishukuru Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo kwa maandalizi ya mafunzo elekezi, akiahidi kutekeleza majukumu yake kwa weledi na kujituma.

DKT. MWINYI AWEKA MSISITIZO WA MAADILI NA UWAJIBIKAJI KWA WALIMU AJIRA MPYA BUSOKELO



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo, Dkt. Mwinyi Mwingi akizungumza na walimu wapya ajira mpya wakati wa ufunguzi wa mafunzo elekezi yaliyofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, tarehe 26 Februari, 2026.

Walimu ajira mpya wakifuatilia kwa makini hotuba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo wakati wa mafunzo elekezi yaliyofanyika katika Halmashauri hiyo tarehe 26 Februari, 2026 kabla ya kuripoti katika vituo vyao vya kazi.



Walimu ajira mpya wakifuatilia kwa makini hotuba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo wakati wa mafunzo elekezi yaliyofanyika katika Halmashauri hiyo tarehe 26 Februari, 2026 kabla ya kuripoti katika vituo vyao vya kazi.

WATUMISHI WA TSC WASHIRIKI MAFUNZO YA USIMAMIZI WA NYARAKA NA KUMBUKUMBU NJOMBE

Na mwandishi wetu – Njombe.

Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wameshiriki kikao kazi na mafunzo maalum ya usimamizi wa nyaraka na kumbukumbu yaliyoandaliwa na Tanzania Records & Archives Management Professional Association (TRAMPA) mkoani Njombe.

Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea washiriki uelewa wa kina kuhusu kanuni, taratibu na mbinu bora za kisasa katika usimamizi wa nyaraka, uhifadhi wa kumbukumbu na matumizi sahihi ya taarifa kwa mujibu wa sheria za utumishi wa umma.

Aidha, washiriki walipata fursa ya kujifunza juu ya umuhimu wa mifumo ya kidijitali katika kurahisisha upatikanaji wa taarifa na kuongeza uwazi katika utendaji kazi wa taasisi.

Watumishi wa TSC walioshiriki mafunzo hayo ni Dorcas Shuma kutoka ofisi za Tume Wilaya ya Monduli, Irene Mndewa (Chamwino), Ernest Kaji (Ilala) na Dorisi Shayo (Tanga).

Washiriki hao wametoa shukrani kwa Katibu wa TSC, Wakurugenzi pamoja na Menejimenti yote ya Tume kwa kuwapatia nafasi ya kushiriki mafunzo hayo muhimu, wakieleza kuwa ni uwekezaji mkubwa katika kuboresha utendaji kazi na kuimarisha misingi ya uwajibikaji ndani ya Tume.

Aidha, wameahidi kutumia maarifa na stadi walizozipata kuboresha mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu katika maeneo yao ya kazi na kuendelea kuitumikia Tume kwa weledi, uadilifu na kwa kuzingatia



Watumishi wa Tume walioshiriki kikao kazi na mafunzo maalum ya usimamizi wa nyaraka na kumbukumbu yaliyoandaliwa na Tanzania Records & Archives Management Professional Association (TRAMPA) mkoani Njombe hivi karibuni.

Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

Ushiriki wa watumishi hao unatarajiwa kuleta mchango chanya katika kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu na kuongeza tija katika utoaji wa huduma ndani ya Tume ya Utumishi wa Walimu.



Watumishi wa Tume walioshiriki kikao kazi na mafunzo maalum ya usimamizi wa nyaraka na kumbukumbu yaliyoandaliwa na Tanzania Records & Archives Management Professional Association (TRAMPA) mkoani Njombe hivi karibuni.

TSC Yaanza Kuamua Rufaa za Walimu kwa Kutumia TSCMIS

Na Mwandishi Wetu – Morogoro

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) katika kuamua rufaa za walimu, hatua inayolenga kuboresha utoaji wa huduma kwa njia ya kidijitali na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

Hatua hiyo imeanza kutekelezwa kupitia majaribio yaliyofanyika wakati wa Mkutano wa Tume uliofanyika hivi karibuni mjini Morogoro, ambapo wajumbe wakiongozwa na Mwenyekiti wa Tume, Prof. Masoud Hadi Muruke, walipitia na kuamua rufaa kwa kutumia mfumo huo.

Akizungumza katika Mkutano huo, Prof. Muruke alisema matumizi ya TSCMIS yanaonesha mafanikio makubwa katika kurahisisha utendaji kazi na kuboresha utoaji wa huduma kwa walimu.

"Tumekuwa tukitumia mfumo wa TSCMIS katika masuala mbalimbali yanayohusu walimu. Leo tumepiga hatua nyingine muhimu katika kushughulikia rufaa za walimu kupitia mfumo. Huu ni mwendelezo mzuri wa matumizi ya teknolojia katika kushughulikia masuala ya walimu. Mfumo huu unasaidia kuokoa gharama, hususan matumizi ya karatasi, na kuongeza ufanisi wa kazi," alisema.

Alifafanua kuwa kupitia mfumo huo, walimu wanaweza kuwasilisha rufaa zao bila kulazimika kusafiri kwenda ofisi za Tume, jambo linalookoa muda na gharama.

Aidha, alisisitiza kuwa mfumo huo hautumiki tu katika kushughulikia mashauri ya nidhamu na rufaa, bali hushughulikia masuala mbalimbali ya kiutumishi ikiwa ni pamoja na usajili wa walimu, upandishwaji vyeo, ubadilishaji wa vyeo, ushughulikiaji wa malalamiko pamoja na kuboresha mawasiliano na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma.

Kupitia mfumo huo mwalimu anaweza kufuatilia maendeleo ya rufaa au huduma anayohitaji kwa wakati. Tume itaendelea kuimarisha usimamizi ili kupunguza au kuondoa kabisa upotevu wa nyaraka.

Hatua hiyo inaonesha dhamira ya Tume ya kutumia teknolojia ya kisasa katika kuboresha huduma na kumrahisishia mwalimu upatikanaji wa huduma kwa haraka na ufanisi zaidi.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kushoto) akiongoza mkutano wa Tume uliofanyika hivi karibuni mjini Morogoro. Pambeni yake ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (katikati) akiongoza mkutano wa Tume uliofanyika hivi karibuni mjini Morogoro. Pichani, upande wa kulia ni Makamu Mwenyekiti wa Tume, Bi. Bahati Mgongolwa na upande wa kushoto ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.

TSC Yaanza Kuamua Rufaa za Walimu kwa Kutumia TSCMIS



Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu wakizwa katika mkutano wa Tume uliofanyika hivi karibuni mjini Morogoro.



Mkutano wa Tume ukiendelea mjini Morogoro hivi karibuni.

TSC Yaanza Kuamua Rufaa za Walimu kwa Kutumia TSCMIS



Mkutano wa Tume ukiendelea mjini Morogoro hivi karibuni.

SERIKALI YAAJIRI WALIMU 454 WILAYANI MPANDA

Na Mwandishi Wetu – Mpanda

Jumla ya walimu 454 wameajiriwa, kusajiliwa na kuthibitishwa kazini Wilayani Mpanda katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mpanda, Bw. Benson Ng'amilo, wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwatumikia walimu.

Bw. Ng'amilo alisema kuwa kati ya walimu hao, 250 ni wa shule za msingi na 204 ni wa shule za sekondari.

Alifafanua kuwa Serikali imehakikisha walimu wa Wilaya ya Mpanda wanapata haki na stahili zao kwa kushughulikia kero na malalamiko yanayohusu upandishaji wa vyeo pamoja na kubadilishiwa miundo ya utumishi (recategorization) baada ya kujiendeleza kitaaluma.

Kwa mujibu wa Bw. Ng'amilo, hatua hiyo imechangia kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi katika upimaji na mitihani ya kitaifa kwa shule za msingi na sekondari.

Akieleza kuhusu upandishaji wa vyeo, alisema katika mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya walimu 581 walipandishwa vyeo, ambapo 356 ni wa shule za msingi na 225 ni wa shule za sekondari.

Katikamwakawafedha 2022/2023, walimu 511 walipandishwa vyeo, kati yao 426 ni wa shule za msingi na 85 ni wa shule za sekondari.

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, walimu 764 walipandishwa vyeo; walimu 503 wa shule za msingi na 261 wa shule za sekondari. Aidha, mwezi Juni 2024, Serikali ilitoa kibali cha kuwapandisha vyeo walimu waliocheleweshwa, ambapo walimu 10 walipandishwa kwa mserereko na walimu 212 walipandishwa vyeo vinavyofuata.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025, walimu 162 walipandishwa vyeo, wakiwemo 89 wa shule za msingi na 73 wa shule za sekondari.

Vilevile, walimu 179 waliojiendeleza kitaaluma wamebadilishiwa miundo yao ya



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mpanda, Bw. Benson Ng'amilo, akiwa katika mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwatumikia walimu.

utumishi (recategorization), ambapo 153 ni wa shule za msingi na 26 ni wa shule za sekondari. Kuhusu fedha za likizo, alisema walimu hulipwa kulingana na upatikanaji wa fedha katika halmashauri kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu.

Katika hatua nyingine, Bw. Ng'amilo aliishukuru Serikali kwa miongozo mbalimbali iliyotolewa ambayo imewasaidia walimu kuepuka makosa yanayoweza kuhatarisha ajira zao. Alisema hali hiyo imechangiwa na kupungua kwa mashauri ya nidhamu; mwaka wa fedha 2023/2024 kulikuwa na walimu 27 wenye mashauri ya nidhamu, mwaka 2024/2025 walikuwa 15, na mwaka 2025/2026 unaoendelea hadi sasa walimu 10 wana mashauri ya nidhamu.

Alisema ili kuimarisha utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi, Ofisi ya TSC Wilaya ya Mpanda imekuwa ikifanya ziara za mara kwa mara shuleni kwa kushirikiana na Maafisa kutoka Idara ya Elimu ya Awali na Msingi,

Sekondari pamoja na Uthibiti Ubora wa Shule. Katika ziara hizo, walimu hukumbushwa kuzingatia Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu.

Aidha, ofisi hiyo imegawa miongozo ya ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi kwa Walimu Wakuu na Wakuu wa Shule ili kuwasaidia katika usimamizi wa walimu wanaoawaongoza, kwa mujibu wa Kanuni ya 12(3) ya Tume ya Utumishi wa Walimu ya mwaka 2016 inayowatambua kama Mamlaka za Nidhamu katika shule wanazoziongoza.

Aliongeza kuwa walimu wapya walioajiriwa mwaka 2025 wamepewa Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya wanaojiriwa katika Utumishi wa Umma, Tanzania Bara, Toleo Na. 1 la mwaka 2025.

Wilaya ya Mpanda ina jumla ya shule 154, zikiwemo shule za msingi 114 na shule za sekondari 40, ikiwa na jumla ya walimu 1,811; kati yao walimu 1,245 ni wa shule za msingi na 566 ni wa shule za sekondari.

KAMATI YA UTAWALA, FEDHA, UTAFTI NA ELIMU KWA UMMA TSC YAPITIA UTEKELEZAJI WA MIPANGO NUSU MWAKA



Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ya Tume ya Utumishi wa Walimu, Bi. Mariam Mwanilwa, akiongoza kikao kilichofanyika Februari 5, 2026 jijini Dodoma.

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ilifanya kikao chake Februari 5, 2026 jijini Dodoma kwa lengo la kujadili masuala mbalimbali yanayohusu utoaji huduma kwa walimu, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Mkutano wa Tume.

Kikao hicho kiliongozwa na Mwenyekiti wa Kamati, Bi. Mariam Mwanilwa, ambaye alieleza kuwa majadiliano yaliyofanyika yalilenga kuhakikisha mipango na mikakati ya Tume inatekelezwa kwa ufanisi, hususan katika maeneo ya utawala, usimamizi wa fedha, utafiti na elimu kwa umma. Alisisitiza kuwa tathmini ya utekelezaji

wa majukumu kwa kipindi cha nusu mwaka wa fedha 2025/2026 ni muhimu katika kupima mafanikio na kuweka maboresho yanayohitajika.

Katika kikao hicho, taarifa mbalimbali ziliwasilishwa na kujadiliwa, zikiwemo utekelezaji wa masuala ya kiutawala pamoja na utendaji wa Idara na Vitengo vya Tume katika kipindi husika. Wajumbe walipitia kwa kina mwenendo wa matumizi ya rasilimali na namna yanavyochangia katika kuboresha huduma zinazotolewa kwa walimu nchini.

Kikao hicho kimeelezwa kuwa sehemu muhimu ya maandalizi ya Mkutano wa Tume, ambao unatarajiwa kujadili na kufanya maamuzi mbalimbali kuhusu masuala ya utumishi wa walimu nchini.



Katibu wa Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ya Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama, akitoa neno la shukrani wakati wa kuhitimisha kikao cha Kamati hiyo kilichofanyika Februari 5, 2026 jijini Dodoma.

KAMATI YA UTAWALA, FEDHA, UTAFITI NA ELIMU KWA UMMA TSC YAPITIA UTEKELEZAJI WA MIPANGO NUSU MWAKA



Washiriki wa kikao cha Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ya Tume ya Utumishi wa Walimu wakizwa kwenye kikao hicho kilichofanyika Februari 5, 2026 jijini Dodoma.

ELIMU YASAIIDIA KUPUNGUZA MASHAURI YA NIDHAMU KWA WALIMU BUKOMBE

Na Mwandishi Wetu- Bukombe

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Bukombe imefanikiwa kutumia elimu kupitia machapisho mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha kuwa mashauri ya nidhamu kwa walimu yanazidi kupungua.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Afisa wa Tume Wilaya ya Bukombe anayeshughulikia masuala ya Nidhamu ya Walimu, Bw. Manjo Mlengela wakati akielezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika utoaji wa huduma kwa walimu.

Alisema kuwa Miongozo na machapisho mbalimbali ambayo yamekuwa yakitolewa na Serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu kama vile Miongozo wa Walimu

wa Ajira mpya yamesaidia walimu kujua Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wa.

Alisema kuwa katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020, Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Bukombe ilikuwa na mashauri ya kinidhamu 65 wakati mwaka 2021 hadi 2025 mashauri yalipungua na kufikia 24.

Alisema kuwa mafanikio hayo yametokana na Tume ya Utumishi wa Walimu kuendesha ziara ya mafunzo na kufanikiwa kuwafikia walimu 965 wa shule za Msingi na Sekondari.

"Tunaishuru Serikali kwa kuchapisha machapisho kama vile Miongozo kuhusu masuala ya Ajira na Maendeleo ya walimu, Miongozo wa Mafunzo Elekezi kwa walimu wapa wanaojirwa katika utumishi wa umma, Miongozo wa Usimamizi wa Maadili na Nidhamu ngazi za Shule na

Miongozo wa Hatua za Nidhamu na Rufaa kwa walimu, hii yote imesaidia katika kufundishia na kujifunza kwa walimu ili kuzingatia Sheria," alisema.

Kwa upande wa Afisa Ajira wa Tume hiyo wilayani Bukombe Bw. Ndaro alisema kuwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2025, walimu 2,533 walifanikiwa kupandishwa vyeo na Serikali.

Aliongeza kuwa katika kipindi hicho walimu 230 walibadilishiwa muundo baada ya kujiendeleza

Wakati huo huo Baadhi ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Serikali wilayani Bukombe wamesema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imejitahidi kuondoa kero za walimu ikiwemo kucheleweshwa kupandishwa madaraja.

Mkuu wa Shule ya Msingi Boma Mw. Madeleke Masenya Joseph alisema kuwa Serikali imefanya jitihada kubwa sana katika kuhakikisha kuwa walimu wanakuwa katika vyeo wanavyostahili.

Alisema kuwa hivi sasa Serikali imeweka mfumo ambao kila mwalimu anapandishwa kulingana na sifa na kuwa katika Daraja stahiki.

Aidha, Mwl. Joseph aliongeza kuwa Serikali imeboresha miundombinu ya Shule kwa kujenga majengo ya kisasa na kukarabati vyumba vya madarasa



Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Bukombe wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya maohojiano hivi karibuni na Afisa Habari wa Tume Makao Makuu Bw. Tiganya Vincent (hayupo katika picha) kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika utoaji wa huduma kwa walimu. Waliopo kwenye picha ni Ndaro Merumba (katikati), kushoto ni Manjo Mlengela na kulia ni Ngendamenya Magambo



Mkuu wa Shule ya Msingi Boma Mw. Madeleke Masenya Joseph

ELIMU YAS Aidia KUPUNGUZA MASHAURI YA NIDHAMU KWA WALIMU BUKOMBE

ambavyo vilionekana kuwa chakavu na kuwafanya walimu kuwa na mazingira mazuri ya kutoa elimu na wanafunzi kuwa na mazingira ya kujifunza.

Alisema kuwa hatua ya Serikali kuanzisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwenye utoaji elimu yamewasaidia kuwaongezea maarifa wao na wanafunzi wanaowafundisha.

Bw. Joseph alisema kuwa kwa upande wa Mitaala mipya itasaidia kuwajenga wanafunzi kujifunza vitu kulingana na mazingira yanayowazunguka na hivyo kuwa rahisi kwao kujitegemea badala ya kutegemea ajira.

Mwl. Winfrida Deogratius Kitobelo alisema kuwa Serikali imesaidia kuondoa kero ya walimu kwa kukaa katika cheo kimoja kwa muda mrefu hata wengine kufikia miaka 6 hadi 7 kwa kuwapandisha kwa njia ya mserekeo.

Alieleza kuwa hatua hiyo imesaidia kuongeza morali ya kazi kwa walimu waliokuwa na changamoto zinazohusu upandishwaji wa vyeo.

Mwl. Winfrida aliongeza kuwa Serikali imejitahidi kuboresha miundombinu ya kufundishia ya kujifunzia ambayo imesaidia kuondoa mrundikano wa wanafunzi katika Darasa moja nje kiwango



*Mwalimu wa Shule ya Msingi Boma
Mwl. Winfrida Deogratius Kitobelo*

kinachotakiwa.

Aidha, alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita pia imejali makundi yote ya kijamii katika kuhakikisha wanapata elimu kwa kutoa kipaumbe cha kuwapatia chakula Watoto wenye mahitaji maalumu wawapo shuleni.

Alisema kuwa hatua hii imesaidia Watoto wenye mahitaji maalumu kupenda masomo na kujifunza katika mazingira rafiki.

Mwl. Brighton Joseph Tibenda alisema kuwa ikilinganishwa na miaka ya nyuma hivi sasa Serikali inapandisha madaraja walimu kwa kasi na kuhakikisha kuwa kila mwalimu anafikia Daraja analostahili kulingana na kiwango cha elimu yake.

Aliongeza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imejitahidi kuhakikisha kuwa miundombinu inakuwa ya kisasa na inakidhi idadi ya wanafunzi wanaohitajika kwa kila darasa.

Mwl. Martha John alisema kuwa Serikali imeiwezesha shule kuwa na miundombinu ya kisasa na kuwapatia samani ambazo zimesaidia katika ufundishaji wa ujifunzaji.

Alisema kuwa mitaala mipya itasaidia wanafunzi kujitegemea kwa kuwa itawasaidia kuwajenga kujifunza kwa vitenda zaidi kwa kulinga na mazingira halisi yao.



*Mwalimu wa Shule ya Msingi Boma Mwl. Brighton
Joseph Tibenda.*



Mwalimu wa Shule ya Boma Mwl. Martha John

SEKONDARI YA KUTWA MPANDA YAISHUKURU SERIKALI YA AWAMU YA SITA KWA KUSIKILIZA KERO ZAO

Na Mwandishi Wetu – Mpanda

Walimu wa Shule ya Sekondari ya Kutwa Mpanda (Mpanda Day Secondary) katika Wilaya ya Mpanda wameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuboresha maslahi ya walimu na kutatua changamoto zilizokuwa zikiwakabili kwa muda mrefu, hali iliyokuwa ikiathiri morali na ufanisi wa utoaji elimu.

Wakizungumza hivi karibuni kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, walimu hao walisema maboresho yaliyofanyika yameleta mabadiliko chanya katika sekta ya elimu.

Mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Kutwa Mpanda, Mwl. Andrew Charles, alisema uboreshaji wa miundombinu na ajira za walimu wapya umechangia kuongeza ufaulu katika shule mbalimbali.

Alisema hatua hiyo imeboresha mazingira ya kazi kwa walimu na ujifunzaji kwa wanafunzi, ambapo kwa sasa karibu kila darasa lina walimu wa masomo ya sayansi, jambo lililopunguza mzigo wa kazi kwa walimu.

Kwa upande wake, Mwl. Beatrice Kitoi alisema mitaala mipya iliyoanzishwa na Serikali itasaidia kukabiliana na changamoto ya ajira nchini na kuibua vipaji vya watoto ambavyo vingepotea.

“Mitaala hii itawajenga watoto kujifunza kwa vitendo na kuwaandaa kufanya shughuli mbalimbali za kuwaingizia kipato kama kilimo cha bustani, ususi, ujasiriamali na hata ufugaji,” alisema.

Aidha, aliipongeza Serikali kwa kuanzisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utoaji wa elimu, hatua iliyowaongezea maarifa walimu na wanafunzi.

Mwl. Shedrack Chikunda alisema Serikali imefanya kazi nzuri kwa kuimarisha matumizi ya TEHAMA shuleni na kushauri juhudi ziendeleo ili kila shule nchini iwe na somo hilo.

Aliongeza kuwa katika kipindi hiki ambacho matumizi ya Akili Unde (Artificial Intelligence – AI) yanaongezeka kwa kasi, ni muhimu vijana wa Kitanzania kuandaliwa mapema ili waweze kukabiliana na mabadiliko hayo ya kiteknolojia.

Naye Mwl. Duduye Sanzagi aliipongeza Serikali kwa ujenzi wa maabara shuleni hapo, jambo linalowawezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo masomo ya Biolojia, Fizikia na Kemia.

Alisema hatua hiyo imeongeza hamasa kwa wanafunzi kupenda masomo ya sayansi kwa kuwa wanapata uelewa wa kina kupitia majaribio ya vitendo.



Mwl. Andrew Charles wa Shule ya Sekondari ya Kutwa Mpanda.



Mwl. Beatrice Kitoi wa Sekondari ya Kutwa Mpanda.



Mwl. Shedrack Chikunda wa Shule ya Sekondari ya Kutwa Mpanda.

**SEKONDARI YA KUTWA MPANDA YAISHUKURU SERIKALI
YA AWAMU YA SITA KWA KUSIKILIZA KERO ZAO**

Mwl. Duduye Sanzagi wa Shule ya Sekondari ya Kutwa Mpanda.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mpanda, Bw. Benson Ng'amilo, (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya walimu wa Shule ya Sekondari ya Kutwa Mpanda mara baada ya mahojiano kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kurwahudumia walimu.

WAJUMBE WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WAPITISHA MPANGO MKAKATI WA MIAKA MITANO IJAYO

Na Mwandishi Wetu- Morogoro

Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mpango Mkakati wa Tume ya Utumishi wa Walimu wa mwaka 2026/27 hadi 2030/31.

Akizungumza mara baada ya kupitishwa kuhusu maboresho ya Mpango na Mtaalamu kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP), Mwenyekiti wa Tume, Prof. Masoud Muruke aliaagiza kuingizwa kwa mapendekezo ya wajumbe ili Mpango huo usaidie kujibu changamoto mbalimbali zinakabili Tume.

Alisema kuwa kupunguza uhaba wa Ofisi ya Tume ngazi za Wilaya ni vema Mpango huo ukazingatia mahitaji halisi ya Tume kwa rasilimali watu na fedha kwa ajili ya kutoa mazingira mazuri ya kuendelea kuwahudumia walimu wa Shule za Msingi na Sekodari za Umma nchini.

"Hakikisheni shughuli na majukumu yote ya Tume ikiwemo

bajeti ya utekelezaji wake yanaingizwa katika Mpango Mkakati ili kuhakikisha kuwa tunafikia lengo la kuanzishwa kwetu," alisema.

Mtaalamu kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijiji Bw. Benjamin Mwalugeni alisema kuwa baada ya kupata maagizo kutoka Tume mapendekezo yaliyozingatiwa ni pamoja na maboresho kwenye sehemu ya Dira na Dhima ya Taasisi (Vision and Mission) ambapo imeonekana kuwa kuna umuhimu wa kuendelea na zile za awali kwa kuwa bado zinaonesha uhalisia na mahitaji ya wakati ya sasa.

Aliongeza kuwa maboresho mengine yaliyofanyika ni kuongeza sura mpya kwenye Mpango Mkakati huo ambayo ni Sura ya Nne inayoelezea Mpango wa Rasilimali (Resource Plan) kwa kuzingatia Mwongozo mpya wa Uandaaji wa Mipango Mikakati uliotolewa na Tume ya Taifa ya Mipango.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mwl. Paulina

Nkwama alisema kuwa Mpango huo umezingatia halisi na utakuwa mapitio kwa ajili ya kuhakikisha kuwa unatekelezwa kwa kuzingatia mazingira yaliyopo kwa kipindi husika.

Mchumi Elias Malaki alisema kuwa baada ya kukamilika mapitio hayo, Mpango huo utapelekwa katika Ofisi ya Tume ya Mpango kwa ajili ya kupitiwa na baada ya kukabailika utolewe kwa ajili ya matumizi.

Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu walipendekeza kuwa makadirio ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango huo kwenye kipengele cha rasilimali Fedha (Financial Resources) yaendane na uhalisia wa shughuli zinazopangwa kutekelezwa katika kipindi hicho cha Mpango yaani mwaka 2026/27 hadi 2030/31.

Waliongeza kuwa rasimu ya Mpango huo iwasilishwe kwenye mamlaka husika kwa ajili ya kuidhinishwa baada ya kufanyiwa maboresho yaliyopendekezwa.



Mhadhiri kutoka Chuo cha Mipango Bw. Benjamin Mwalugeni akitoa maelezo kwa Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu kuhusu Mpango Mkakati wa Tume wa mwaka 2026/27-30/31 hivi karibuni wakati wa Mkutano wa Tume.

WAJUMBE WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WAPITISHA MPANGO MKAKATI WA MIAKA MITANO IJAYO



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Prof. Masoud Muruke akitoa maagizo kwa Menejimenti ya Tume wakati wa Mkutano wa Tume. Kulia ni Makamu Mwenyekiti wa Tume Bi. Bahati Shabani Mgongolwa.



Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu Bi. Jane Mtindya akitoa taarifa ya Kamati ya Maadili na Nidhamu wakati wa Mkutano wa Tume.



Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu Bw. Lameck Mahewa akitoa taarifa ya Kamati ya Ajira na Maendeleo ya Walimu wakati wa Mkutano wa Tume



MIONGOZO YA SERIKALI YAWAIMARISHA WALIMU WILAYANI TANGANYIKA

Na Mwandishi Wetu – Tanganyika

Miongozo mbalimbali iliyotolewa na Serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeendelea kuwasaidia walimu Wilayani Tanganyika kutambua Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma pamoja na kuimarisha uzalendo katika kutekeleza majukumu yao.

Kauli hiyo imetolewa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Tanganyika, Bw. Reuben Haji Mmbaga, wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano kutoka Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwahudumia walimu.

Bw. Mmbaga alisema kuwa kupitia miongozo hiyo, walimu wameweza kufahamu kwa kina maslahi yao wanapotimiza wajibu wao, yakiwemo haki za likizo, uhamisho, fedha za kujikimu, mipaka ya kazi zao katika Utumishi wa Umma, pamoja na taratibu za kufikisha malalamiko yao kwenye mamlaka husika.

Alieleza kuwa katika kuendelea kuwajengea walimu uelewa na kuwakinga dhidi ya makosa ya kinidhamu, Tume imekuwa ikiendesha vikao vya kila robo mwaka kwa lengo la kujadili na kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili.

Aidha, TSC imekuwa ikiendesha ziara shuleni kwa ajili ya utoaji wa elimu, kufanya vikao na walimu, kutoa mafunzo elekezi kwa walimu wapya na kugawa miongozo mbalimbali, ikiwemo Miongozo wa Mafunzo kwa Walimu Wapya pamoja na ufafanuzi wa Kanuni za Maadili katika Utendaji Kazi kwa Walimu.

Kwa mujibu wa Bw. Mmbaga, ugawaji wa miongozo hiyo umechangia kuimarika kwa nidhamu miongoni mwa walimu na kupunguza mashauri ya kinidhamu yanayowasilishwa Tume, tofauti na kipindi cha nyuma ambapo kulikuwa na kiwango kikubwa cha ukiukwaji wa maadili ya kazi.

Aliishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa

kuajiri walimu 387 wa shule za msingi na sekondari wilayani humo, kupandisha madaraja walimu 32 kwa njia ya mserekeo, pamoja na kulipa malimbikizo ya mishahara kwa walimu 215. Aliongeza kuwa madai ya walimu 71 yako katika hatua za mwisho Hazina kwa ajili ya malipo.

Kwa upande wao, walimu wa Wilaya ya Tanganyika wameipongeza Serikali kwa kuboresha maslahi yao na kutatua changamoto zilizokuwa zikiwakabili kwa muda mrefu, hali iliyorejesha morali na kuongeza ufanisi katika utoaji wa elimu.

Mwalimu wa Shule ya Sekondari Kakoso, Mwl. Lucy Massawe, alisema jitihada za kuhakikisha walimu waliokuwa hawajapandishwa madaraja kwa muda mrefu wanapata stahiki zao sasa zinaonekana wazi.

“Serikali imeweka mfumo unaohakikisha kila mwalimu anapandishwa daraja kulingana na sifa na muda wa utumishi,” alisema.

Aidha, alieleza kuwa uboreshaji wa miundombinu, hususan ujenzi wa mabweni, umechangia kuwaweka wanafunzi karibu na mazingira ya shule na kuongeza utulivu katika masomo yao.

Mwalimu Sharifa Mohamed Issa aliishukuru Serikali kwa kuboresha

huduma za kijamii ikiwemo afya na usafiri, pamoja na kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambayo yamewasaidia walimu kubadilishana uzoefu na kuongeza ubora wa ufundishaji.

“Nchi imepiga hatua kubwa katika miundombinu. Barabara nyingi zimeboreshwa na hivyo kurahisisha utekelezaji wa majukumu yetu,” alisema.

Naye Mwalimu Bwire Mangasa aliipongeza Serikali kwa kutoa vifaa na mafunzo ya TEHAMA shuleni, hatua inayowawezesha walimu na wanafunzi kwenda sambamba na maendeleo ya sayansi na teknolojia duniani.

Kwa upande wake, Mwalimu wa Taaluma wa Shule ya Sekondari Kakoso, Mwl. Frank Josephat Chelango, alisema Serikali imeweka kipaumbele katika maendeleo ya sekta ya elimu kwa kuhakikisha walimu wanapata haki zao kwa wakati, ikiwemo mishahara na madaraja.

Aliongeza kuwa shule hiyo sasa ina maabara tatu za masomo ya Biolojia, Kemia na Fizikia pamoja na vifaa na vitabu vya kutosha, jambo linalochochea ufaulu wa wanafunzi.



Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Tanganyika, Bw. Reuben Haji Mmbaga, akizungumza na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwahudumia walimu.

MIONGOZO YA SERIKALI YAWAIMARISHA WALIMU WILAYANI TANGANYIKA



Mwalimu wa Shule ya Sekondari Kakoso, Mwl. Lucy Massawe, akizungumza wakati wa mahojiano hayo.



Mwalimu wa Shule ya Sekondari Kakoso, Mwl. Sharifa Mohamed Issa, akitoa maoni yake.



Mwalimu wa Shule ya Sekondari Kakoso, Mwl. Bwire Mangasa, akizungumza wakati wa mahojiano.



Mwalimu wa Taaluma wa Shule ya Sekondari Kakoso, Mwl. Frank Josephat Chelango, akieleza mafanikio ya sekta ya elimu.

MIONGOZO YAWAIMARISHA WALIMU NA KUCHOCHEA UZALENDU WILAYANI MLELE

Na Mwandishi Wetu – Mlele

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mlele imetoa elimu kwa walimu 1,080 wa shule za msingi na sekondari za umma kuhusu miongozo mbalimbali ya utumishi, hatua iliyowajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma na kuimarisha uzalendo kwa nchi yao.

Hayo yameelezwa na Afisa wa TSC Wilaya ya Mlele, Bw. Jitihada Amon, wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Tume Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwatumikia walimu.

Bw. Amon alisema mafanikio hayo yametokana na ziara zilizofanyika katika shule 103 wilayani humo, ambapo walimu wenye changamoto mbalimbali walitambuliwa na kuwasiliana na mwajiri pamoja na Maafisa Elimu (Msingi na Sekondari) ili kuboresha maslahi yao.

Alieleza kuwa sambamba na ziara hizo, Tume imegawa miongozo na kutoa mafunzo yaliyowasaidia walimu kufahamu haki na wajibu wao, tofauti na ilivyokuwa hapo awali. Hatua hiyo imechangia kupungua

kwa mashauri ya kinidhamu kutoka wastani wa walimu watatu kwa mwaka hadi wastani wa walimu wawili kwa mwaka.

Aidha, TSC imekuwa ikiandaa mikutano ya walimu katika kanda mbalimbali za wilaya hiyo kwa ajili ya kuwapatia elimu kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma, pamoja na kuendesha vipindi maalumu vya redio kutoa elimu kwa walimu, ikiwemo kupitia Redio Mpimbwe FM.

Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025, Bw. Amon alisema Serikali imefanikiwa kupandisha vyeo walimu 736, kuwabadilishia kada walimu 72 waliojiendeleza kitaaluma, na kuthibitisha kazini walimu 305.

Wakati huo huo, walimu wa Wilaya ya Mlele wameipongeza Serikali kwa kuboresha maslahi yao na kutatua changamoto zilizokuwa zikiwakabili kwa muda mrefu, hatua iliyorejesha morali na kuongeza ufanisi katika utoaji wa elimu.

Mwalimu wa Shule ya Sekondari Usevya, Mwl. Andrew Samson Mwakalobo, alisema jitihada za kuhakikisha walimu waliochelewa kupandishwa madaraja wanapata stahiki zao sasa zinaonekana wazi.

Alibainisha kuwa tangu mwaka 2021 amepandishwa madaraja mara mbili kutokana na mfumo unaozingatia sifa na muda wa utumishi.

Aidha, alisema uboreshaji wa miundombinu kupitia ujenzi wa shule mpya umesaidia kupunguza mrundikano wa wanafunzi. Pia alipongeza kuanzishwa kwa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utoaji wa elimu, hatua inayowaongezea maarifa walimu na wanafunzi.

Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari Usevya, Mwl. Michael Mwakibete, aliishukuru Serikali kwa kumtatulia changamoto ya kukaa muda mrefu katika daraja moja, ambapo sasa amepandishwa mara mbili na anatarajia kupandishwa tena mwaka 2027.

Aliongeza kuwa ajira za walimu wapa zimepunguza mzigo wa kufundisha wanafunzi wengi darasani, huku ujenzi wa madarasa na vyoo ukiboresha mazingira ya kujifunzia. Pia alisema uanzishwaji wa mitaala mipya na mafunzo ya amali umeongeza hamasa ya wanafunzi kujifunza na kuibua vipaji vyao.

Naye Mwalimu wa Shule ya Sekondari Usevya, Mwl. Sabas Mkorongo, alisema mfumo bora wa mawasiliano kati ya walimu na Maafisa Elimu wa Wilaya na Mkoa umeimarisha utekelezaji wa majukumu yao.

Alisema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imejitahidi kuhakikisha kila mwalimu anapata haki zake kwa wakati na kupandishwa daraja stahiki, tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Kwa upande wake, Mwalimu Sengo Amos Karova aliishukuru Serikali kwa kuboresha maslahi ya walimu, ikiwemo nyongeza za mishahara na upandishaji wa madaraja yaliyokuwa yamesimama kwa muda mrefu.

Alisema matumizi ya TEHAMA yamerahisisha ufundishaji na ujifunzaji kwa kuwawezesha walimu kutafuta na kuandaa mada kwa urahisi, hatua iliyochangia kuimarika kwa ufaulu wa wanafunzi.



Afisa wa TSC Wilaya ya Mlele, Bw. Jitihada Amon.



Mwalimu wa Shule ya Sekondari Usevya, Mwl. Andrew Samson Mwakalobo.

MIONGOZO YAWAIMARISHA WALIMU NA KUCHOCHEA UZALENDU WILAYANI MLELE



Mwalimu wa Shule ya Sekondari Usevya, Mwl. Andrew Samson Mwakalobo.



Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari Usevya, Mwl. Michael Mwakibete



Mwalimu wa Shule ya Sekondari Usevya, Mwl. Sabas Mkorongo



Mwalimu Sengo Amos Karova

KAMATI YA MAADILI NA NIDHAMU TSC YAJIPANGA KUIMARISHA UZINGATIAJI WA SHERIA KWA WALIMU

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Kamati ya Maadili na Nidhamu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ilifanya kikao chake Februari 6, 2026 jijini Dodoma ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Mkutano wa Tume, kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa maadili na nidhamu katika kada ya ualimu nchini.

Kikao hicho kilifanyika katika ukumbi wa mikutano wa Tume na kuongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mwl. Jane Mtindya, ambaye alisisitiza umuhimu wa kuendelea kuweka mifumo madhubuti ya kusimamia mwenendo wa walimu ili kuhakikisha taaluma ya ualimu inalindwa na kuenziwa.

Akizungumza wakati wa kikao, Mwl. Mtindya alieleza kuwa maadili

na nidhamu ni nguzo kuu katika utumishi wa walimu, kwani mwalimu ni kioo cha jamii na ana wajibu wa kuishi na kutenda kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu.

Alibainisha kuwa Kamati itaendelea kushauri na kusimamia utekelezaji wa mikakati itakayosaidia kuimarisha uwajibikaji na weledi katika sekta ya elimu.

Katika kikao hicho, wajumbe walijadili mikakati mbalimbali ikiwemo kuimarisha ufuatiliaji wa mashauri ya kinidhamu, kuongeza uelewa wa walimu kuhusu taratibu za kazi, na kuboresha mifumo ya kushughulikia malalamiko kwa wakati ili kuleta haki na uwazi.

Aidha, Kamati ilipokea na kupitia taarifa ya rufaa mbalimbali za walimu

zilizokuwa zimeandaliwa kwa ajili ya kuwasilishwa katika Mkutano wa Tume kwa uamuzi. Hatua hiyo ni sehemu ya mchakato wa kuhakikisha haki inatendeka kwa kuzingatia misingi ya kisheria na kiutumishi.

Katibu wa Kamati hiyo, Mwl. Paulina Nkwama, alisisitiza umuhimu wa maandalizi ya kina katika uchambuzi wa rufaa hizo ili Tume iweze kufanya maamuzi yenye tija, yanayolinda maslahi ya walimu na kuimarisha nidhamu kazini.

Kwa ujumla, kikao hicho ni sehemu muhimu katika kusimamia kwa karibu maadili na nidhamu ya walimu, kwa lengo la kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa uadilifu, weledi na kwa kuzingatia sheria na taratibu za utumishi wa umma.



Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili na Nidhamu ya Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Jane Mtindya, akiongoza kikao kilichofanyika Februari 6, 2026 jijini Dodoma.

KAMATI YA MAADILI NA NIDHAMU TSC YAJIPANGA KUIMARISHA UZINGATIAJI WA SHERIA KWA WALIMU



Washiriki wa kikao cha Kamati ya Maadili na Nidhamu ya Tume ya Utumishi wa Walimu wakijadili mikakati ya kuimarisha nidhamu kwa walimu tarehe 6 Februari, 2026 jijini Dodoma.

WALIMU WA SHULE YA MSINGI KASHAULILI WILAYANI MPANDA WAISHUKURU SERIKALI KWA KUTATUA KERO ZAO

Na Mwandishi Wetu – Mpanda

Baadhi ya walimu wa Shule ya Msingi Kashaulili iliyopo katika Manispaa ya Mpanda wameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutatua kero zilizokuwa zikiwakabili kwa muda mrefu.

Wakizungumza hivi karibuni kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, walimu hao walisema hatua zilizochukuliwa zimeongeza ari na utulivu katika utendaji wao wa kazi.

Mkuu wa Shule ya Msingi Kashaulili, Mwl. Mnasa James, aliishukuru Serikali kwa kuruhusu walimu kuanza tena kupandishwa madaraja baada ya kusimamishwa kwa muda mrefu.

Alisema jitihada hizo zinaonesha kuwa Serikali inathamini mchango wa walimu na sekta ya elimu kwa ujumla katika maendeleo ya taifa, jambo linalodhihirika pia kupitia uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya shule.

Mwl. James aliongeza kuwa Serikali imerahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali kwa walimu, ikiwemo mikopo na likizo kupitia Mfumo wa ESS, hatua iliyoondoa foleni na urasimu uliokuwepo hapo awali.

Kwa upande wake, Mwl. Benjamin Masai alisema Serikali imejitahidi kuweka mazingira mazuri kwa watumishi wa umma kuipenda kazi yao.

“Serikali imekuwa sikivu kwa watumishi wa umma, wakiwemo walimu, kwa kuhakikisha inapandisha madaraja walimu wote waliostahili. Hata mimi ni miongoni



Mkuu wa Shule ya Msingi Kashaulili, Mwl. Mnasa James, akizungumza wakati wa mahojiano kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwatumikia walimu.

mwa wanufaika wa jitihada hizo. Kwa kweli ninaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita,” alisema.

Aliongeza kuwa upatikanaji wa vifaa vya kufundishia umechangia kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi kila mwaka.

Mwl. Masai pia alieleza kuwa Serikali imeanzisha mifumo ya TEHAMA, ikiwemo TSCMIS, unaomwezesha mwalimu kufahamu lini atapandishwa daraja na hata tarehe ya kustaafu.

Naye Mwl. Benard Gama aliipongeza Serikali kwa kushughulikia changamoto za ucheleweshaji wa upandishaji madaraja zilizokuwepo miaka ya nyuma.

Alisema kupandishwa kwa mishahara na madaraja kwa njia

ya kawaida na ile ya mserereko kumeleta utulivu na kuboresha maisha ya walimu.

Mwalimu Doris Kuyasiwa alisema uboreshaji wa miundombinu ya shule umeongeza mvuto wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia, hali iliyochangia kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya msingi pamoja na kuimarika kwa ufaulu.

Aliongeza kuwa matumizi ya TEHAMA yamewasaidia walimu kupata mada na rejea katika nakala laini kupitia tovuti mbalimbali za umma kwa ajili ya kufundishia.



Mwl. Benjamin Masai wa Shule ya Msingi Kashaulili.

WALIMU WA SHULE YA MSINGI KASHAULILI WILAYANI MPANDA WAISHUKURU SERIKALI KWA KUTATUA KERO ZAO



Mwl. Benard Gama na Mwl. Doris Kuyasizwa wa Shule ya Msingi Kashaulili.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mpanda, Bw. Benson Ng'amilo (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya walimu wa Shule ya Msingi Kashaulili mara baada ya mahojiano.

WALIMU WA MPANDA WAISHUKURU SERIKALI YA AWAMU YA SITA KWA KUSIKILIZA KERO ZAO

Na Mwandishi Wetu – Mpanda

Walimu wa Shule ya Msingi Ilembo katika Wilaya ya Mpanda wameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuboresha maslahi yao na kutatua changamoto zilizokuwa zikiwakabili kwa muda mrefu, hali iliyokuwa ikiathiri morali na ufanisi katika utoaji wa elimu.

Wakizungumza hivi karibuni kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, walimu hao walisema hatua zilizochukuliwa zimeleta mabadiliko chanya katika sekta ya elimu.

Mkuu wa Shule ya Msingi Ilembo, Mwl. Neema Omolo Abwao, alisema Serikali imejitahidi kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa walimu kwa kushughulikia kero mbalimbali zilizokuwa zikijitokeza.

“Serikali hii kwa kweli imesikia kilio chetu kwa kupandisha madaraja walimu wote wanaostahili, kulipa mishahara kwa wakati na kuweka mfumo wa kupata mikopo bila urasimu, hivyo kuwaepusha walimu na mikopo kausha damu iliyokuwa ikiwanyima utulivu baadhi yao,” alisema.

Aliongeza kuwa tangu shule hiyo ilipoanzishwa mwaka 1952, haikuwa na umeme, lakini Serikali ya Awamu ya Sita imefanikisha kuwekewa miundombinu ya umeme, jambo lililoboreshwa mazingira ya kazi na ujifunzaji.

Kwa upande wake, Mwl. Anna Kayumba alisema uboreshaji wa miundombinu pamoja na ajira mpya za walimu umeongeza ufanisi katika ufundishaji ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Alieleza kuwa matumizi ya TEHAMA yamewasaidia walimu kujiongezea ujuzi na kubadilishana uzoefu kuhusu mada mbalimbali,

hali inayowanufaisha wanafunzi katika kupata elimu bora.

Naye Mwl. Issa Kibona alisema Serikali imeboresha sekta ya elimu katika Wilaya ya Mpanda kwa kujenga madarasa 18 katika Shule ya Msingi Kasisiwe, hatua iliyosaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani.

Aidha, alisema Serikali imetoa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, ikiwemo vitabu na vishikwambi, vinavyowawezesha walimu kutafuta taarifa na marejeo kupitia tovuti mbalimbali za Serikali kwa ajili ya kuimarisha ufundishaji.

Mwl. Tabu Paza naye aliipongeza Serikali kwa kuwapatia vitabu vipya, ikiwemo vya somo la Kiswahili vyenye maudhui ya nyimbo za uzalendo.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuwajenga wanafunzi katika misingi ya uzalendo tangu wakiwa wadogo, kuwahamasisha kuipenda nchi yao na kuepuka kushawishika na maneno ya uchochezi.



Mkuu wa Shule ya Msingi Ilembo, Mwl. Neema Omolo Abwao, akiwa katika mahojiano na Afisa wa Kitengo cha Mawasiliano Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kurwatumikia walimu.

WALIMU WA MPANDA WAISHUKURU SERIKALI YA AWAMU YA SITA KWA KUSIKILIZA KERO ZAO



Mwl. Anna Kayumba wa Shule ya Msingi Ilembo akiwa katika mahojiano na Afisa wa Kitengo cha Mawasiliano Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita.



Mwl. Issa Kibona wa Shule ya Msingi Ilembo akiwa katika mahojiano na Afisa wa Kitengo cha Mawasiliano Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita.

Mwl. Tabu Paza wa Shule ya Msingi Ilembo akiwa katika mahojiano na Afisa wa Kitengo cha Mawasiliano Makao Makuu kuhusu mafanikio hayo



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mpanda, Bw. Benson Ng'amilo (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya walimu wa Shule ya Msingi Ilembo mara baada ya mahojiano hayo.

WALIMU WA SHULE YA MSINGI MPANDANDOGO WAISHUKURU SERIKALI YA AWAMU YA SITA

Na Mwandishi Wetu – Mpanda

Walimu wa Shule ya Msingi Mpandandogo, Wilaya ya Tanganyika, wameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuboresha maslahi yao na kutatua changamoto zilizokuwa zikiathiri utendaji wao.

Wakizungumza kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita, walisema maboresho yaliyofanyika yameongeza morali na ufanisi katika utoaji wa elimu.

Mwalimu Maximilian Ismaili alisema Serikali imeboresha miundombinu kwa kujenga madarasa mapya na vyoo, hatua iliyoweka mazingira bora ya kujifunzia.

Mwl. Ally Msangi aliipongeza Serikali kwa ajira mpya za walimu na uboreshaji wa miundombinu uliosaidia kupunguza msongamano darasani na kuongeza ufanisi wa ufundishaji.

Aliongeza kuwa matumizi ya TEHAMA pamoja na upatikanaji wa vitabu na vishikwambi vimewasaidia

walimu na wanafunzi kupata maarifa kupitia tovuti mbalimbali za Serikali.

Mwl. Samwel Fyula alisema TEHAMA imewawezesha walimu na wanafunzi kupata maarifa kwa urahisi na kuongeza uelewa wa masomo.

Naye Mwl. Doris Ndejambi aliishukuru Serikali kwa kutoa miongozo inayowaelimisha walimu kuhusu stahili zao, mavazi yanayotakiwa na Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Utumishi wa Walimu.



Bw. Reuben Haji Mmbaga akiwa katika picha ya pamoja na walimu wa Shule ya Msingi Mpanda Ndogo baada ya mahojiano.

WALIMU WA SHULE YA MSINGI MPANDANDOGO WAISHUKURU SERIKALI YA AWAMU YA SITA



Walimu wa Shule ya Msingi Mpandandogo wakizungumza wakati wa mahojiano kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu